**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA PILI

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA PILI

**27 JANUARI, 2016**

## MKUTANO WA PILI

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA PILI - TAREHE 27 JANUARI, 2016

**I. DUA:**

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Job Ndugai (Spika) alisoma Dua na kukiongoza kikao.

MAKATIBU MEZANI:
1. Ndg. John Joel
2. Ndg. Ramadhani Issa
3. Ndg. Asia Minja
4. Ndg. Zainabu Issa

**II. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, aliapa kiapo cha uaminifu mbele ya Spika.

**III. MASWALI:**

Maswali yafuatayo yaliulizwa na waheshimiwa wabunge:-

**1. OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na. 16: Mhe. Boniventura Destery Kiswaga

Swali la nyongeza: Mhe. Boniventura Destery Kiswaga

Swali Na 17: Mhe. Mgumba Tebweta Omary

Swali la nyongeza: Mhe. Mgumba Tebweta Omary

**2. OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Swali Na. 18: Kwa niaba ya Mhe. Hafidhi Ally Tahir,

Mhe. James Mbatia aliuliza swali hili.

Nyongeza:

1. Mhe. James Francis Mbatia
2. Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe
3. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia
4. Mhe. Hafidhi Ally Tahir

3. **WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:**

   Swali Na 19: Mhe. Khatib Said Haji

   Swali la nyongeza: 1. Mhe. Khatib Said Haji

4. **WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

   Swali Na. 20: Mhe. Hamidu Hassan Bobali

   Swali la nyongeza: 1. Mhe. Hamidu Hassan Bobali

   Swali Na. 21: Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa

   Swali la nyongeza: 1. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa

   2. Mhe. Zitto Kabwe Zuberi

5. **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASAILIANO:**

   Swali Na. 22: Mhe. Peter Ambrose Lijualikali

   Swali la nyongeza: 1. Mhe. Peter Ambrose Lijualikali

6. **WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

   Swali Na. 23: Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

   Swali la yongeza: Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

   Swali na 24: Mhe. Deo Kaseyenda sanga

   Swali nyongeza: Mhe. Deo Kaseyenda Sanga

7. **WIZARA YA FEDHA NA MPANGO:**

   Swali Na. 25: Mhe. Masoud Abdallah Salim

   Swali la nyongeza: Mhe. Masoud Abdallah Salim

Swali Na. 26: Mhe. Hawa Mchafu Chakoma

Swali la nyongeza: Mhe. Hawa Mchafu Chakoma

8. **WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

Swali Na. 27: Mhe. Lolesia jeremiah Bukwimba

Swali la yongeza: Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

Swali Na: 28 Mhe. John John Mnyika - swali liliulizwa kwa niaba na Mhe. James Francis Mbatia

Swali la yongeza: Mhe. James Francis Mbatia

9. **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Swali Na. 29: Mhe. Gimbi Dotto Masaba

Swali la nyongeza: Mhe. Gimbi Dotto Masaba

**IV. MATANGAZO:**

1. Wageni mbalimbali waliokuwepo Bungeni walitambulishwa.
2. Kamati ya bajeti kukutana saa 7 mchana katika Ukumbi wa Msekwa C.
3. Utawala – Mazishi ya Oscar Mtenda – Wabunge wanaopenda kushiriki wajiandikishe mapema.
4. NIDA wameomba radhi kuwa hawataweza kuendesha zoezi la kuwaandikisha Waheshimiwa Wabunge kwa leo.
5. Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile ameomba Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam wakutane baada ya kuahirisha Kikao.
6. Mhe. Waziri Mwigulu Lameck Nchemba anaomba kukutana na Wabunge wanaotoka Mikoa inayolima kahawa na korosho.

## V. MIONGOZO YA SPIKA:

1) Mhe. Juma Ahmad Ngwali aliomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7), 63 na 64(1)(a) kuhusu jibu la Waziri wa Habari kwamba alisema uwongo kuwa TFF ni suala la Muungano wakati TFF haihusiki Zanzibar.

   Spika aliahidi kutoa majibu ya suala hilo baadae.

2) Mhe. Saed Ahmed Kubenea alitumia Kanuni 68(7) kuzungumzia suala la hilohilo la Mhe. Waziri wa Habari kuifanya TFF ni sehemu ya Muungano wakati Wazanzibar hawaruhusiwi hata kugombea nafasi yoyote ya uongozi.

   Spika aliahidi kutoa majibu ya suala hilo baadae.

3) Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara alitumia Kanuni ya 68(7) na 44(1) na (2) kuomba mwongozo juu ya uulizwaji wa maswali ya nyongeza kwamba kwa nini Waziri kajibu maswali matatu badala ya mawili.

   Spika alitumia Kanuni ya 5 kumwambia Mbunge kwamba kilichofanyika ni halali.

4) Mhe. Susan Limbweni Kiwanga aliomba mwongozo kutumia Kanuni ya 47(1) ili Bunge lijadili jambo la dharula kuhusu wananchi wanaoishi kuzunguka Bonde la mto Kilombero kwa kuwa sasa hawalimi hivyo karibu vijiji 126 vitakumbwa na njaa.

## VI. KAULI ZA MAWAZIRI:

Mhe. Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Utamaduni , Wasanii na Michezo alitoa kauli ya Serikali kuhusu TBC kusitisha urushaji wa matangazo ya moja kwa moja ya Bunge(*Live broadcasting*).

- Baada ya Kauli ya Serikali kutolewa Spika alitoka kitini, Mhe. Andrew John Chenge (Mwenyekiti) aliliongoza Bunge na kuendelea na majadiliano ya Hotuba ya Rais. Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto alisimama na kutoa Hoja kwa kutumia kanuni ya 69 kwamba mjadala uhairishwe ili Bunge lijadili kauli ya Waziri wa Habari, jambo lililozua utata na fujo na Mhe. Halima Mdee kuibuka na Hoja ya Haki za Bunge kupitia Kanuni ya 55 iliyozua utata na kupelekea Mwenyekiti wa Bunge asitishe shughuli za Bunge kwa muda wa saa moja ili kuipa nafasi kamati ya Uongozi kukutana na kushauri kuhusu suala hilo.

Bunge lilisitishwa saa 5:30 asubuhi.

## VII. BUNGE KUREJEA:

Bunge lilirejea saa 6:30 mchana na Mhe. Andrew John Chenge [Mwenyekiti] alitoa Taarifa kwamba Kamati ya Uongozi baado inaendelea na Kikao hivyo alisitisha tena Shughuli za Bunge hadi saa 10:00 jioni.

## VIII. BUNGE KUREJEA:

Bunge lilirejea saa 10:00 jioni na Mhe. Andrew John Chenge aliyeongoza Kikao alitoa maelezo kuhusu suala la Mhe. Zitto Ruyagwa Kabwe, Wabunge wa Upinzani hawakuridhika na maelezo hayo na kusababisha kuomba miongozo bila kufuata utaratibu jambo lililopelekea kuwe na fujo ndani ya ukumbi, Kiti kiliwasihi waachwe fujo wanazofanya lakini walikataa kutii amri hiyo.

Mwenyekiti aliamua kutumia kanuni ya 76(1) kusitisha Shughuli za Bunge kwa muda ili kumpa nafasi Mpambe wa Bunge kudhibiti fujo hizo.Wabunge hao walitolewa nje na askari chini ya usimamizi wa mpambe wa Bunge

- Baada ya utulivu kurudia Bunge lilirejea, Mwenyekiti alielezea kwamba suala la kambi ya Upinzani na Wabunge wa vyama vingine kuleta fujo atlipeleka kwenye kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili kamati hiyo iweze kushauri Bunge kuhusu adhabu ili inayostahili kutolewa kwa Wabunge.

## IX. HOJA ZA SERIKALI:

Hoja ya Waziri Mkuu kwamba Bunge lilijadili Hotuba ya Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la kumi na moja tarehe 20, Novemba, 2015, majadiliano yaliendelea na waheshimiwa Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia.

**MWONGOZO KUHUSU HOJA YA MHE. ZITTO RUYAGWA KABWE:**

1. Kwa mujibu wa Kanuni 52(2) baada ya Spika kuruhusu Hoja ya kujadili Hotuba ya Rais, Mbunge yeyote binafsi hataruhusiwa kutoa Hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge wala kuuliza swali.

2. Kwa mujibu wa kanuni ya 51 hakuna haki yoyote ya Bunge iliyovunjwa kwa mujibu wa Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge.

3. Hoja iliyo mbele ya Bunge ya Hotuba ya Rais, mjadala wake uendelee kama ulivyopangwa kwenye Orodha ya Shughuli za siku hiyo.

**Uchangiaji uliendelea…**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 29. | Mhe. Innocent Lugha Bashungwa | – | CCM |
| 30. | Mhe. Juliana Daniel Shonza | – | CCM |
| 31. | Mhe. Mussa Rashid Ntimizi | – | CCM |
| 32. | Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako | – | CCM |
| 33. | Mhe. Costantine John Kanyaswi | – | CCM |
| 34. | Mhe. John Peter Kadutu | – | CCM |
| 35. | Mhe. Elibariki Emanuel Kingu | – | CCM |
| 36. | Mhe. Flatei George Massay | – | CCM |
| 37. | Mhe. Hasna Sudi Mwilima | – | CCM |
| 38. | Mhe. Almasi Athumani Maige | – | CCM |
| 39. | Mhe. Peter Joseph Serukamba | – | CCM |
| 40. | Mhe. Njalu Daudi Silanga | – | CCM |
| 41. | Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo | – | CCM |
| 42. | Mhe. Ally Seif Ungando | – | CCM |
| 43. | Mhe. Joseph Kasheku Musukuma | – | CCM |

**Tangazo**: Kampuni ya uwekezaji (UTT) ipo hapa Bungeni kuanzia tarehe 26 – 29 Januari hivyo Wabunge waitembelee ili kupata Elimu ya uwekezaji pamoja na miradi inayoendeshwa na Taasisi hiyo.

## X. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE:

Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Andrew John Chenge aliahirisha Shughuli za Bunge saa 1:45 jioni hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

**DODOMA**
**27 JANUARI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**